

Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki

Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki ni nini?

Tao la Mashariki ni safu ya Milima ya kale iliyofunikwa na Misitu yenye unyevu pamoja na mbuga katika nchi za Tanzania na Kenya.

Wanasayansi wanaamini kwamba misitu iliyoko Milima ya Tao la Mashariki imekuwepo kwa zaidi ya miaka milioni 30.

Milima ya Tao la Mashariki inapatikana katika wilaya 14 kama ifuatavyo:

Pare Kusini/Kaskazini	- Same na Mwangi
Usambara Magharibi/Mashariki	- Muheza, Lushoto na Korogwe
Nguu	- Kilindi
Nguru	- Mvomero
Uluguru	- Morogoro na Mvomero
Ukaguru	- Kilosa
Rubeho	- Mpwapwa na Kilosa
Malundwe	- Morogoro
Udzungwa	- Kilombero, Mufindi na Kilolo
Mahenge	- Ulanga

Inakadiriwa kuwa karibu kilomita za mraba 5,000 ya misitu ndizo zilizosalia kwenye milima.

Sifa za Misitu ya Tao la Mashariki ni zipi?

Maelfu ya aina mbalimbali za mimea na wanyama wanapatikana katika misitu hii pekee na si mahali pengine popote duniani. Hii inajumuisha angalau aina 100 za ndege, mamalia (wanyama wanaonyonyesha), wanyama jamii ya vyura, na jamii ya nyoka na mijusi. Vilevile kuna aina kama 800 za mimea na idadi kubwa ya viumbe wadogo wadogo kama vipepeo na jamii ya majongoo.

Zaidi ya asilimia 70 za uoto wa misitu zimeharibiwa

Ramani ya Milima ya Tao la Mashariki



Uhifadhi wa Tao la Mashariki

Uhifadhi wa maeneo yaliyobaki ya misitu na mbuga za majani ya Tao la Mashariki ni muhimu kwa jamii ya kimataifa na Tanzania kwa ujumla.

Maeneo mengi ya misitu yamepotea ndani ya kipindi cha miaka 100, kwa sababu ya upanuzi wa maeneo ya kilimo, ukataji miti ovyo na uchomaji moto.

Eneo kubwa ya Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki lipo chini ya uhifadhi wa serikali kuu au halmashauri za wilaya. Hata hivyo eneo hili linakabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa fedha na watumishi kuendesha shughuli za uhifadhi.

Tangu mwaka 1998, wananchi wakisaidiwa na vyama vya kiraia wamekuwa wakijihusisha zaidi katika usimamizi wa Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki. Haya ni mabadiliko makubwa sana katika sera ya usimamizi wa Misitu.

Mradi wa Uhifadhi na Usimamizi wa Misitu ya Tao la Mashariki (CMEAMF)

Mradi wa Uhifadhi na Usimamizi wa Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki (CMEAMF) unalenga kuboresha mipango ya muda mrefu ya usimamizi endelevu ya misitu hii. Mradi unaratibiwa na serikali ya Tanzania, kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii - Idara ya Misitu na Nyuki. Unachangiwa kiushauri na mashirika mawili yasiyo ya Kiserikali- CARE Tanzania na Kikundi cha Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG).

Mfuko wa Uhifadhi Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) ni sehemu muhimu ya mradi na unalenga kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya shughuli za uhifadhi.

Mradi huu wa CMEAMF unafadhiliwa na GEF-UNDP.

Misitu ya milima hii ina manufaa gani kwa Tanzania?

MAJI

Angalau asilimia 25 ya watazania wanategemea Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki kwa upatikanaji wa maji.

Mito ya Wami, Kilombero, Ruvu, Zigi, Ruaha na Pangani yote inatiririka kutoka miinuko ya maeneo mbalimbali katika Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki na ina manufaa makubwa kwa jamii za vijijini na kwa shughuli za kilimo kwenye maeneo ya mabondeni. Kwa mfano, Mto Ruvu unaotoa maji kwa mji wa Dar es Salaam unatiririka kutoka Milima ya Uluguru na Mto Zigi unaotoa maji kwa mji wa Tanga unatiririka kutoka Milima ya Usambara Mashariki.

UMEME

Nishati ya umeme inayotumia maji kutoka Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki inachangia asilimia 50 ya nishati ya

umeme wa Taifa.

CHAKULA


Hali ya hewa na mandhari nzuri iliyoko katika Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki inawezesha kilimo cha aina mbalimbali za mazao, mboga na matunda, kwa ajili ya jamii husika na hata kuuzwa katika miji mbalimbali hapa Tanzania.

Chakula kinacholimwa katika Milima ya Tao la Mashariki na kuuzwa katika miji mbalimbali kinachangia kwa kiasi kikubwa katika kulisha jamii za mijini, kuinua kipato kwa jamii hizi za wakulima na hatimaye kupunguza umaskini nchini Tanzania.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:



Mradi wa Uhifadhi na Usimamizi wa Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki
S.L.P. 289, Morogoro,
Simu: 023 3082 Simu pepe: 023 3084
Barua pepe: easternarc@easternarc.or.tz



Mkurugenzi Mtendaji
Mfuko wa Uhifadhi Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki,
S.L.P. 6053, Morogoro
Simu: 023 3660 Simu pepe: 023 3113
Barua pepe: eamcef@easternarc.or.tz
www.easternarc.or.tz



Kikundi cha Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG)
S.L.P. 23410, Dar es Salaam,
Simu: 022 2669007,
Barua pepe: tfcg@tfcg.or.tz
www.tfcg.org